

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

24 MEI, 2024



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU TAREHE 24 MEI, 2024

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA
BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

426. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya katika Kata ya Maguliwa ambapo Wananchi wameshakamilisha ujenzi wa Boma.

427. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mkakati gani wa Serikali kuongeza wigo wa barabara za lami katika Wilaya ya Kigamboni.

428. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI CHAUREMBO (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Mfereji wa Shegho ambao unaathiri Wakazi wa Kata ya Kiburugwa Jimbo la Mbagala.

WIZARA YA NISHATI:

429. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi waliopisha Mradi wa umeme Kakono - Misenyi.

430. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itamaliza mgao wa umeme unaokatika kila Jumanne na Alhamisi katika Jimbo la Kilombero.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

431. MHESHIMIWA JONAS WILLIAM MBUNDA (MBINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itajenga jengo la kisasa la Mahakama ya Wilaya ya Mbinga.

WIZARA YA UJENZI:

432. MHESHIMIWA PROF. PALAMAGAMBA JOHN AIDAN MWALUKO KABUDI (KILOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Chanzuru hadi Melela - Kilosa.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

433. MHESHIMIWA NAJMA MURTAZA GIGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kwa nini Serikali isiweke kwenye Mitaala somo la uraia na uzalendo ili kizazi kijacho kiwe na uelewa wa haki na wajibu wa raia nchini.

434. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini majengo ya Chuo cha VETA Chikundi – Ndanda yataanza kutumika.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**435. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA
KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha mbegu ya Ng'ombe ya asili ya Ufipa haipotei.

WIZARA YA AFYA:

**436. MHESHIMIWA CONCHESTA LEONCE
RWAMLAZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kwa nini Kada zinazoweza utendaji kazi katika Hospitali hazijumuishwi pindi ajira zinapotangazwa.

WIZARA YA MAJI:

**437. MHESHIMIWA MAIMUNA AHMAD PATHAN (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mikoa ya Lindi na Mtwara itapata Mradi mkubwa wa Maji kutoka Mto Rufiji ambao upo jirani.

WIZARA YA FEDHA:

**438. MHESHIMIWA ABDI HIJA MKASHA
(MICHEWENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurejesha huduma za Kibenki za CRDB, NMB na PBZ katika Wilaya ya Micheweni.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA
24 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**